

ORS (Solution de Réhydratation Orale – Serum ya kukunywa) kwa alama ya Ebola

Leta dawa ya SRO MARA MOJA ikiwa utaona alama yoyote ya Ebola:



Moto



Kutapika



Kuhara


Namna gani kuleta SRO kwa njia nzuri



Changanya paquet 1 ya SRO katika chungu nusu (demi pots) 3 (litres 1) ya maji safi ya kunywa.



Mwaga muchanganyiko kwa kopo (ao chupa). Kuwa mwangalifu ili uepuke kugusa kopo, chupa au vitu vingine ya mgonjwa. USIGAWANYE SRO, kopo ao chupa na wengine.



- Tia moyo watoto na watu wazima kukunywa SRO mara mingi ikiwa wanahara au kutapika.
- Weka SRO ile haijatumika ndani ya kitu kilichofunikwa vizuri.
- Tupa kila siku SRO ile haikutumiwa.
- Acha kutumia SRO wakati kuhara na kutapika inaacha.